# HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI INJ. EVARIST NDIKILO KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA DR. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI TAREHE 28 JUNI, 2020 WILAYANI KISARAWE

***Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

***Mhe. Waziri wa Maji,***

***Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, (Mb Kisarawe),***

***Katibu Mkuu Wizara ya Maji,***

***Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Pwani,***

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa,***

***Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,***

***Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe,***

***Wakuu wa Taasisi mbalimbali za Serikali ngazi ya Taifa na Mkoa,***

***Viongozi wa Dini,***

***Wanahabari,***

***Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana,***

***Wananchi Wenzangu,***

***Aslaam Aleikum, Bwana Yesu asifiwe, Tumsifu Yesu Krito.***

**Mhe. Rais,**

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Afya njema na kutukutanisha hapa leo kwenye Ziara yako ya siku moja Mkoani Pwani ya kuzindua Mradi wa Maji wa Kibamba hadi Kisarawe. Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Pwani nikukaribishe sana hapa Kisarawe wewe binafsi pamoja na Msafara wako. Aidha, tunawakaribisha wageni wote mliotoka nje ya Mkoa wetu, Karibuni sana.

**Mhe. Rais,**

Hali ya Mkoa wa Pwani ni Salama, Wananchi wanaendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo kama kawaida. Kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Pwani naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano unayoiongoza kwa namna ambavyo umewezesha Mkoa wetu wa Pwani kupiga hatua kubwa katika Sekta mbalimbali, Mfano; Afya, Viwanda, Nishati (Umeme), Kilimo (Korosho na Ufuta), Elimu, Maji n.k. Pwani ya mwaka 2015 ni tofauti kabisa na Pwani ya mwaka 2020 katika nyanja zote. Kwa sababu ya muda naomba nizungumzie Sekta ya Maji kwa kuwa leo upo hapa kuzindua Mradi wa Maji wa Kibamba – Kisarawe. Taarifa ya kina ya Miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelezwa katika Mkoa wa Pwani imewasilishwa kwa wasaidizi wako mapema kwa ajili ya kumbukumbu ya ziara hii.

**Mhe. Rais,**

Tarehe 20-22 Juni 2017 ulifanya Ziara katika Mkoa wetu. Pamoja na mambo mengine ulizindua Mtambo wa kusukuma Maji kutoka Mlandizi kwenda Dar es Salaam. Katika salamu zangu za Mkoa, Nilitoa ombi kwako la Wilaya ya Kisarawe kupatiwa huduma ya Maji Safi na Salama. Mhe. Rais, nakumbuka ulielekeza DAWASA kupeleka Maji katika Wilaya ya Kisarawe. Nashukuru sana kwa kutukubalia ombi letu, kwani tangu kuanzishwa kwa Wilaya ya Kisarawe ni katika kipindi cha Utawala wako, Wilaya ya Kisarawe imepata Maji Safi na Salama kwa ajili ya matumizi ya Majumbani na Viwandani (Domestic and Industrial use). Maji haya yametokana na upanuzi wa Mtambo wa kusukuma Maji wa Mlandizi (Ruvu Juu).

Kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Kisarawe na Mkoa wa Pwani kwa ujumla, nitumie nafasi hii kukushukuru sana. Aidha, niwapongeze DAWASA kwa kutekeleza vema na kwa wakati maelekezo yako. Mradi huu wa kutoa Maji Kibamba hadi Kisarawe (Kilometa 17) uliogharimu **Shilingi Bilioni 10.6** umekamilika kwa **asilimia 100.**

**Mhe. Rais,**

Kukamilika kwa mradi huu kumefanya Wananchi wa Wilaya ya Kisarawe kupata huduma ya Maji Safi na Salama, hivyo kuepukana na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa Maji Safi na Salama, kumeondoa adha ya Wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta Maji (kumtua mama ndoo kichwani). Vilevile kwa Watanzania waliokuwa wanahofia kuishi Kisarawe kutokana na ukosefu wa huduma ya Maji Safi na Salama sasa wanapakimbilia kuishi na kufanya Wilaya ya Kisarawe kukua

kwa kasi katika Nyanja mbalimbali. Kwa uwezo wa Mtambo wa kusukuma Maji kutoka Kibamba kuja Kisarawe ni lita milioni 6 kwa siku wakati matumizi ya wakazi wa Kisarawe kwa saa ni lita milioni 1.2 faida nyingine ya mradi huu ni kivutio muhimu kwa wawekezaji wa Viwanda hasa katika eneo la Viwanda la Visegese.

**Mhe. Rais,**

**Hali ya upatikanaji wa Maji Mkoa wa Pwani.**

Hadi kufika mwezi Mei, 2020 katika Mkoa wa Pwani upatikanaji wa huduma ya Maji Safi na Salama kwa wakazi waishio Vijijini umefikia **asilima 66.6** na kwa wakazi waishio Mjini umefikia **asilimia 88.**

**Mhe. Rais,**

kukamilika kwa Miradi mbalimbali inayotekelezwa na DAWASA na RUWASA katika Mkoa itapelekea kukaribia au kufikia lengo la upatikanaji wa Maji Kitaifa hadi ifikapo Oktoba 2020 ambalo ni **asilimia 85** Vijijini na **asilimia 95** Mijini.

**Mhe. Rais,**

Halmashauri zinazohudumiwa na DAWASA ni sita (6) ambazo ni Halmashauri za Wilaya za **Bagamoyo, Chalinze, Kibaha Vijijini, Kisarawe, Mkuranga na Halmashauri ya Mji Kibaha.** Halmashauri ambazo hazihudumiwi na DAWASA ni tatu (3) pekee ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Mafia na Rufiji. Niwapongeze DAWASA na Wizara ya Maji, kwa kufanya kazi kubwa Mkoa wa Pwani.

**Mhe. Rais,**

Ipo miradi Mikubwa saba ikiwamo na huu wa Kisarawe inayotekelezwa na DAWASA katika jitihada za kuhakikisha Mkoa wetu unapata Maji Safi na Salama na pia DAWASA inachangia katika kuhamasisha uwekezaji wa Viwanda katika Mkoa wa Pwani. Miradi hiyo ni kama ifuatayo:-

i. Mradi wa Maji Kongowe hadi Kiwanda cha TANCHOICE na Eneo la Viwanda Soga, Mradi huu umekamilika na umegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.1** na unategemewa kunufaisha Kiwanda kikubwa cha kuchakata nyama ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchinja Ng'ombe 1,000, Mbuzi na Kondoo 4,500 kwa siku. Bomba hili litahudumia pia Wananchi katika njia litakayopita.

ii. Mradi wa Maji Visiga madafu hadi eneo la Viwanda Zegereni, mradi huu upo katika hatua ya usanifu na unagharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.3.** Mradi huu unatarajiwa kuanza kutekelezwa Julai 1, 2020 na utahudumia pia Wananchi wengi katika njia utakapopita

iii. Mradi wa Maji Mlandizi – Chalinze hadi eneo la Viwanda Mboga, Mradi huu sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 73**, ambapo kwa sasa hatua inayoendelea ni ulazaji wa mabomba. Mradi huu utagharimu **Shilingi Bilioni 17.1.**

iv. Mradi wa Maji Ruvu Chini – Kiwangwa hadi Msata. Mradi huu upo katika hatua ya usanifu, na utaanza Julai 1, 2020.

v. Mradi wa upanuzi wa Chanzo cha Maji Wami. Mradi huu upo katika hatua ya awali ya usanifu. Kukamilika kwa upanuzi wa chanzo cha Wami utasaidia upatikanaji wa uhakika wa huduma ya Maji Safi na Salama kwa Vijiji vya Mandela, Miono, Mkange, Mdaula, Ubena pamoja na Vijiji vya Morogoro na Tanga.

vi. Mradi wa Maji Mkuranga: Mradi huu unahusisha Ujenzi wa Tenki lenye ujazo wa Lita milioni 1.5, ujenzi wa Kisima pamoja na ulazaji wa bomba kilometa 65 ambao tayari umekamilika. Mradi huu utagharimu **Shilingi Bilioni 5.6.** Mradi huu umekamilika kwa asilimia 80 na ni utekelezaji wa ahadi yako wakati wa Kampeni za Uchaguzi mwaka 2015.

vii. Mradi wa Maji Kisiwa cha Jibondo Wilayani Mafia: Wizara ya Maji imegharimia Mradi huu. Mradi huo umekamilika na umegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.1.** Kukamilika kwa mradi huo kumeondoa changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma ya Maji Safi na Salama katika Kisiwa cha Jibondo Wilayani Mafia. Eneo hili halijawahi kupata maji Safi na Salama tangu Uhuru. Awamu ya Tano ya Serikali yako imefikisha Maji kwenye Kisiwa hiki chenye idadi ya watu 2,432.

viii. Katika Ziara yako Mkoani Pwani, ulisimama katika eneo la Ikwiriri Wilayani Rufiji ambapo uliahidi upatikanaji wa Maji katika mradi wa Maji Ikwiriri. Ulitoa maelekezo kwa DAWASA kununua na kufunga Pampu za Maji. Napenda kukupa taarifa kuwa maelekezo yako

yametekelezwa na Wananchi wa eneo hilo wanapata huduma ya Maji Safi na Salama.

ix. Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) imepata **Shilingi Bilioni 2.4** kutoka katika mfuko wa Maji kwa ajili ya upanuzi wa Miradi ya Maji na kuanzisha Miradi mipya katika Wilaya 5 za Kibiti, Rufiji, Kisarawe, Kibaha na Bagamoyo. Tayari **Shilingi Milioni 840** zimeshatumika katika miradi mbalimbali na kazi zinaendelea kwa kutumia mfumo wa "FORCE ACCOUNT".

**Mhe. Rais,**

Ukijumlisha miradi yote hii katika Mkoa wa Pwani utaona wazi kwamba tutafikia lengo la upatikanaji Maji Kitaifa kwa Vijijini **asilimia 85** na Mijini **asilimia 95.**

**Mhe. Rais,**

Tunalo eneo la Viwanda la Visegese hapa Kisarawe. Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe imetenga takribani eneo lenye ukubwa wa ekari 1,000 Visegese kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda. Hadi sasa DAWASA wamelaza bomba lenye urefu wa kilometa 4 kuelekea eneo la Viwanda Visegese. Hata hivyo bado kilometa 3 kufikisha Maji katika eneo hilo. Maombi ya Mkoa kwa DAWASA ni kuharakisha ukamilishaji wa Mtandao wa kupeleka Maji katika eneo hilo la uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi. Hadi sasa eneo hilo lina Viwanda 5 ambavyo vinategemea Maji kutoka DAWASA.

**Maombi ya Mkoa kwa Mhe. Rais,**

**Mhe. Rais,** Naomba nimalize Hotuba yangu kwa kuwasilisha maombi machache (maombi mawili tu).

Tuna changamoto ya Barabara kutoka Kiluvya (Morogoro Road) hadi Mpuyani (Kisarawe) yenye urefu wa Kilometa 19.04 ambayo ni kiungo muhimu na njia fupi kutoka Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya ya Kisarawe, Mkuranga na maeneo mengine ya jirani. Kwa sasa Barabara hii ni ya tabaka la changarawe ambayo inahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Barabara hii imepita eneo la Viwanda la Visegese, lakini kutokana na aina ya Barabara ilivyo ya changarawe, ukomo wa uzito uliopo ni tani 10 hali inayofanya magari ya mizigo kutoka maeneo hayo ya Viwanda kwenda Mikoani kulazimika kupitia Dar es salaam.

Ombi langu kwako Mhe. Rais ni Barabara hii kujengwa kwa kiwango cha Lami, ili kuruhusu magari yenye uzito mkubwa kupita ili kuepusha mzunguko mrefu wa kupitia Dar es salaam pia kujengwa kwa Barabara hii kutaunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya za Kisarawe, Mkuranga, Kibiti na Rufiji.

**Mhe. Rais,**

Changamoto nyingine ni ya Barabara ya kutoka TAMKO (Morogoro Road) hadi Mapinga Bagamoyo, yenye urefu wa kilometa 23. Ni kiungo muhimu kati ya Makao Makuu ya Mkoa na Bagamoyo. Kilometa 3 ni za Lami na kilometa 20 ni za changarawe. Maombi yetu ni kujengwa kilometa 20 kwa kiwango cha Lami ikiwemo na fedha za fidia kwa Wananchi takribani **Shilingi Bilioni 8.**

**Mhe. Rais,**

Barabara hiyo ni njia fupi kutoka Makao Makuu ya Mkoa kwenda Wilayani Bagamoyo na maeneo mengine ya Mkoa wa Dar es salaam. Kujengwa kwa kiwango cha Lami kwa Barabara hiyo kutasaidia Wananchi katika shughuli za kibiashara na huduma za kijamii.

**Mhe. Rais,** kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha.

Inj. Evarist Welle Ndikilo

**MKUU WA MKOA WA PWANI**